NSW GOVERNMENT

School counselling service

Information for parents and carers

# Huduma ya shule ya ushauri nasaha

## Maelezo kwa wazazi na walezi

Shule zote za umma za NSW zinapata usaidizi wa kisaikolojia kupitia huduma ya ushauri ya shule.

Huduma ya ushauri ya shule inajumuisha washauri nasaha wa shule na wanasaikolojia wa shule ambao wanatoa ushauri nasaha, tathmini ya kisaikolojia na huduma za maingilio kwa wanafunzi kuanzia chekechea hadi Mwaka wa 12. Wanashughulikia pamoja na familia, wafanyakazi wa shule, na wataalumu wengine ili kusaidia mahitaji ya kujifunza, afya ya akili na ustawi ya wanafunzi, na kuunda mazingira ya kujifunza yenye salama, afya, na kusaidika.

Wafanyakazi wote wa ushauri wa shule wana sifa za baada ya kuhitimu katika saikolojia na hutumia utaalamu wao katika afya ya akili, kujifunza, na tabia kuwasaidia watoto na vijana kufanikiwa kielimu, kijamii, kitabia, na kihisia.

Mshauri nasaha wa shule au mwanasaikolojia wa shule anaweza:

- kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi
- kutathmini mahitaji ya wanafunzi ya kujifunza na ya afya ya akili
- kufanya kazi kwa ushirikiano na walimu na wafanyakazi wataalumu
- kusaidia familia kuelewa na kusimamia mahitaji ya watoto ya kujifunza na ya afya ya akili
- kuwasiliana na mashirika ya nje na wataalamu wa afya ya akili ili kutoa usaidizi ulioratibiwa, wa pande zote kwa wanafunzi binafsi.

Wakati wanapofanya kazi na wanafunzi, wazazi au walezi, na walimu, wafanyakazi wa shule wa ushauri nasaha wataeleza jinsi wanavyofanya kazi, kusikiliza kwa makini kile kinachosemwa,kusaidia kufafanua chaguo na kuhimiza kufanya maamuzi kwa ufahamu.

## Usiri

Wafanyakazi wa ushauri wa shule hutoa usaidizi wa kisaikolojia wa hiari na wa siri kwa wanafunzi. Maelezo ya siri hayatashiriki na wengine bila ruhusa ya mwanafunzi, mzazi, au mlezi isipokuwa yakihitajika na sheria au kuzuia hatari kubwa kwa usalama au ustawi njema.

## Rufaa

Vipaumbele vya usaidizi wa ushauri nasaha shuleni huamuliwa kwa kushauriana na timu za kujifunza na ustawi wa shule. Wazazi au walezi ambao wana wasiwasi kuhusu kujifunza, afya ya akili na/au ustawi wa mtoto wao wanaweza kuomba miadi kwa kuwasiliana na shule. Wanafunzi wanaweza pia kujielekeza au kutafuta usaidizi kutoka kwa wazazi au waalimu ili kupanga miadi.

## Huduma ya wakalimani wa simu

Ikiwa unataka maelezo tafadhali piga simu shuleni. Ikiwa unamhitaji mkalimani kukusaidia na swali lako, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Wakalimani wa Simu kwa 131 450 na umwombe kwa mkalimani katika lugha yako.

Umwambie mpigaji simu (mwendeshaji) ile nambari ya simu unayotaka kupiga simu na mpigaji simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.